

Mwanafunzi mwenye ugonjwa wa Narcolepsy na Mfumo wa Elimu

504 VS. IEP: MTOTO WAKO ANAHITAJI NINI?

Kifungu cha 504: Sheria ya Mabadiliko

- Sheria ya Haki za Kiraia inayotoa ulinzi dhidi ya ubaguzi; Sheria ya Marekebisho ya Ujuzi
- Inatoa mpango wa jinsi mtoto atakavyoweza kufikia mazingira ya kujifunzia
- Mabadiliko katika mazingira ya kujifunzia ili kuweka usawa wa fursa kwa wote
- Mwanafunzi anaweza kuendelea kupokea huduma hizi hata baada ya elimu ya sekondari, katika elimu ya juu

Ustahiki: 1) Mtoto ana ulemavu wa kimwili au kiakili unaoathiri kwa kiasi kikubwa shughuli moja au zaidi muhimu za maisha, 2) ana rekodi ya kuwa na ulemavu huo au 3) anachukuliwa kuwa na ulemavu wa aina hiyo.

Mpango wa Elimu Uliobinafsishwa

- Sheria ya Shirikisho Kuhusu Elimu Maalum; Sheria ya Elimu ya Watu wenye Ulemavu (IDEA)
- Inatoa mpango wa elimu maalum kwa mtoto shuleni
- Inatoa huduma za elimu maalum na huduma zinazohusiana ambazo zimebinafsishwa ili kukidhi mahitaji ya kielimu ya mtoto
- Zitasitishwa pale mwanafunzi atakapohitimu au kufikia kikomo cha umri wa elimu ya msingi na sekondari (K-12)

Ustahiki: 1) Mtoto anayetambulika kuwa na ulemavu mmoja au zaidi kati ya aina 13 maalum za ulemavu zilizoordheshwa chini ya IDEA na 2) ulemavu huo unaathiri utendaji wa kielimu na/au uwezo wa kujifunza na kufaidika na mtaala wa elimu ya jumla.

Walimu wanaojua jinsi ya kukabiliana na dalili za Narcolepsy wanaweza kushawishi kwa njia chanya jinsi wanafunzi wenzake na wafanyakazi wanavyomtendea mwanafunzi aliye na Narcolepsy.

Narcolepsy ni maradhi ya usingizi yatoakanayo na nyurolojia ambayo hayana tiba ambapo ubongo unashindwa kudhibiti mizunguko ya kawaida ya kulala na kuamka. Haitambuliwi ipasavyo na mara nyingi haigunduliwi kwa wakati. Watoto mara nyingi hugunduliwa kimakosa kuwa na ADHD, msongo wa mawazo, matatizo ya tabia, kukosa pumzi wakati wa usingizi, na matatizo mengine ya afya ya akili, kabla ya kugunduliwa kwa usahihi kuwa wana Narcolepsy.



PO Box 60293
Worcester, MA 01606
www.wakeupnarcolepsy.org



MAHITAJI

- Usimwadhibu mwanafunzi kwa kuchelewa kufika
- Ruhusu mwanafunzi apumzike kwa muda mfupi (dakika 20-30) darasani au eneo maalum
- Usimwamshe mwanafunzi endapo atalala darasani
- Mruhusu mwanafunzi kusimama, kutembea, au kunywa maji, jambo linaloweza kuzuia asilale
- Kagua kama mwanafunzi ameelewa na ruhusu mwanafunzi wenzie kumwandikia notisi, kupata notisi na mihadhara iliyorekodiwa kutoka kwa mwalimu
- Usimweke mwanafunzi darasani wakati wa mapumziko kwa ajili ya kazi, anahitaji kutembea tembea na kuamka
- Punguza kazi na majukumu ya darasani mara tu mwanafunzi anapoonyesha kuwa ameelewa somo
- Panga muda wa kufanya mtihani wakati ambao mwanafunzi huwa macho zaidi, na ruhusu mapumziko na muda wa kulala
- Mruhusu mwanafunzi kuchagua sehemu ya kukaa/kozi
- Shirikiana na ofisi ya watu wenye ulemavu (kwa wanafunzi wa chuo)

Kwa msaada wa shule, mwanafunzi mwenye Narcolepsy anaweza kufanikiwa.



Walimu katika shule za awali, msingi, na sekondari (K-12) na vyuo wanapaswa kuelewa kuwa mtoto mwenye Narcolepsy sio mvivu. Wahakikishe kuwa mahitaji yanayofaa yanatolewa darasani pamoja na kwenye mitihani ya kitaifa, wilaya na chuo na kutoa msaada kwa familia kupitia uchunguzi unaohusiana na matumizi ya dawa, usingizi na tabia ya mtoto.

Utafiti unaonyesha kuwa usingizi wa mchana wa kupindukia wa muda mrefu (EDS) kwa watoto wa umri wa shule huathiri:

- Utendaji wa Kielimu
- Matatizo ya Nidhamu
- Mahusiano ya Kifamilia/Rika
- Kuanzisha/Kudumisha Urafiki
- Ustawi wa Kihisia na Uwezo wa Kudhibiti Hisia
- Ushiriki wa Mtoto katika Shughuli za Shule
- Ushiriki katika Elimu/Michezo
- Uchaguzi wa Taaluma
- Uwezo wa Kudumisha Ajira
- Afya ya Kimwili na Usalama